


# kuku wa kienyeji

## je, uzalishaji unakidhi soko?



**Warsha ya Tano ya Wakulima wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini**
iliyofanyika Mbeya,
Tarehe 2 – 4 Desemba 2002



TARP II - SUA Project

# KUKU WA KIENYEJI: JE UZALISHAJI UNAKIDHI SOKO?

Warsha ya Tano ya Wakulima wa
Kanda ya Nyanda za Juu Kusini
Iliyofanyika Ukumbi wa Vijana Wakatoliki, Mbeya

Desemba 2-4, 2002

**Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania**

***(TARP II-SUA Project)***

Desemba 2002

*Imeandikwa na*

Bw. A. Bakari
Dk. J. G. Lyimo-Macha
Prof. E. K. Batamuzi

*Na Kuharíriwa na*

Wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji wa Mradi

| | |
|---|---|
| Prof. L. D. B. Kinabo - | Mratibu |
| Prof. R. E. Malimbwi - | Mjumbe |
| Prof. A. J. P.Tarimo - | Mjumbe |
| Dk. P. J. Makungu - | Mjumbe |

**ISBN: 9987 – 650 – 74 - 5**

*Kimechapishwa na:*

Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima
Wadogowadogo Tanzania (TARP II-SUA Project)
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo
SLP 3151
Morogoro
Simu: +255 23 2600970 au +255 23 2603511 ext. 1102

Toleo namba: TS 2 - 59

# YALIYOMO


| | | | |
|---|---|---|---|
| | **Dibaji** | | **v** |
| | **Vifupisho** | | **vii** |
| **1.0** | **Utangulizi** | | **1** |
| | 1.1 | Madhumuni ya warsha | 1 |
| | 1.2 | Washiriki wa warsha | 1 |
| | 1.3 | Ufafanuzi wa maneno | 2 |
| | 1.4 | Matarajio ya washiriki | 3 |
| | 1.5 | Mbinu zilizotumika | 4 |
| **2.0** | **Hali ya uzalishaji wa kuku wa kienyeji** | | **4** |
| | 2.1 | Umuhimu wa kuku wa kienyeji | 5 |
| | 2.2 | Sababu zinazosababisha kuku wa kienyeji asithaminiwe | 6 |
| | 2.2.1 | Matatizo na kipaumbele cha utatuzi kwa mujibu wa wakulima wanawake | 7 |
| | 2.2.2 | Matatizo na kipaumbele cha utatuzi kwa mujibu wa wakulima wanaume | 8 |
| | 2.2.3 | Matatizo na kipaumbele cha utatuzi kwa mujibu wa wagani | 8 |
| | 2.2.4 | Matatizo na kipaumbele cha utatuzi kwa mujibu wa NGOs | 9 |
| | 2.2.5 | Matatizo na kipaumbele cha utatuzi kwa mujibu wa watafiti | 10 |
| **3.0** | **Mapendekezo ya namna ya kuinua thamani ya kuku wa kienyeji katika kuchangia pato la kaya** | | **11** |
| | 3.1 | Mapendekezo ya wakulima wanaume | 11 |
| | 3.2 | Mapendekezo ya wakulima wanawake | 12 |
| | 3.3 | Mapendekezo ya wagani | 14 |
| | 3.4 | Mapendekezo ya NGOs | 16 |
| | 3.5 | Mapendekezo ya watafiti | 17 |

| | | |
|---|---|---|
| **4.0** | **Maazimio ya warsha** | **19** |
| **5.0** | **Tathmini ya warsha** | **19** |
| **6.0** | **Kufunga warsha** | **20** |
| **7.0** | **Viambatisho** | **21** |
| | Namba 1: Orodha kamili ya washiriki wa warsha | 21 |
| | Namba 2: Shughuli muhimu ambazo washiriki wanajishughulisha nazo katika maisha ya kila siku | 23 |
| | Namba 3: Michoro ya chapati kuonesha shughuli za washiriki wa warsha | 24 |
| | Namba 4: Ahadi za utekelezaji wa maazimio ya warsha | 29 |
| | Namba 5: Ushauri wa kitafiti juu ya kuku wa kienyeji | 35 |
| | Namba 6: Matarajio ya washiriki | 36 |

# DIBAJI

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula, na Chuo Kikuu cha Norway cha Kilimo, kinatekeleza mradi wa Utafiti wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania. Mradi huu ambao ulianza rasmi mwezi Septemba 2000, unagharamiwa na Serikali ya Norway kupitia Shirika lake la Maendeleo (NORAD).

Kati ya shughuli muhimu zilizopangwa ili kutekeleza malengo ya mradi na kuimarisha uhusiano na wakulima, watafiti na washauri wa wakulima ni kufanya warsha zenye madhumuni yafuatayo:

1. Kuwajumuisha watafiti, wakulima na washauri wa kilimo ili kudadisi kuhusu mambo muhimu yanayohitaji kushirikishwa pande zote kwa lengo la kufanikisha kilimo na ufugaji
2. Kuchambua na kuainisha matatizo yanayowakabili wakulima wadogowadogo
3. Kupanga ili kutambua mambo gani yapewe uzito au kipaumbele zaidi
4. Kushiriki katika kupeana uzoefu wa maeneo muhimu ya kilimo na mifugo.

Chapisho hili linawasilisha Mwenendo wa Warsha ya tano ya Wakulima wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kuhusu Uzalishaji wa Kuku wa Kienyeji, iliyofanyika katika ukumbi wa Mikutano, wa Vijana Wakatoliki, Mbeya, Desemba 2-4, 2002. Mwenendo wa warsha umechapishwa na kutolewa katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

*L. D. B. Kinabo*
*Mratibu wa Mradi*

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ARI | Taasisi ya Utafiti wa Kilimo |
| CDFT | Mfuko wa Maendeleo ya Jamii |
| IFAD | Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo |
| NAEP | Programu ya Taifa ya Ushauri wa Kilimo |
| NGO | Shirika lisilo la Kiserikali |
| NLH | Chuo Kikuu cha Norway cha Kilimo |
| RTD | Radio Tanzania Dar es salaam |
| SUA | Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo |
| TARP II | Mradi wa Taifa wa Utafiti wa Kilimo Awamu ya Pili |
| UNDP | Shirika la Umoja wa Mataifa la Mipango ya Maendeleo |

# 1.0 UTANGULIZI

## 1.1 Madhumuni ya warsha

Warsha iliandaliwa na Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania (TARP II SUA) unaotekelezwa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula pamoja na Chuo Kikuu cha Norway cha Kilimo (NLH). Lengo kuu la warsha lilikuwa ni kubaini sababu zinazofanya uzalishaji wa kuku wa kienyeji kutokidhi mahitaji ya soko na kubuni mbinu za kukabiliana nazo ili mkulima aweze kuongeza uzalishaji wa kuku wa kienyeji na anufaike na soko lililopo la kuku wa kienyeji. Warsha ilikuwa na madhumuni mahsusi yafuatayo ili kufanikisha lengo hilo:

i. Kuainisha mtazamo wa makundi yaliyowakilishwa katika warsha juu ya uthamani wa kuku wa kienyeji na jinsi wanavyojishughulisha nao.
ii. Kubaini tofauti iliyopo kati ya mtazamo wa sasa kuhusu uzalishaji wa kuku wa kienyeji na mtazamo ambao ungepaswa kuwapo kulingana na msukumo wa soko ulivyo. Kubaini matatizo yanayosababisha kuwepo kwa tofauti hiyo na kuyapatia kipaumbele.
iii. Kupendekeza mbinu na mikakati itakayowezesha kumfanya kuku wa kienyeji kuwa na hadhi na thamani inayostahili.

## 1.2 Washiriki wa warsha

Jumla ya washiriki 35 walihudhuria katika warsha hiyo na mchanganuo wao ni kama ifuatavyo; wakulima wanawake (9), wakulima wanaume (8), wataalamu wa ugani (4), watafiti (10), wawakilishi wa mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) (3) na mwezeshaji (1).

Washiriki walitoka mikoa ya Iringa, Mbeya, Ruvuma, na Rukwa katika kanda ya Nyanda za Juu Kusini. Watafiti walitokea taasisi za SUA, Morogoro na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (ARI) Uyole,

Mbeya. Mashirika yasiyo ya kiserikali yaliyowakilishwa ni ADP Isangati Trust Fund, Community Development Trust Fund (CDTF) Songea, Intermón Oxfam, Tanzania (Morogoro) na Ileje Rural Development Trust Fund. Orodha ya washiriki pamoja na anuani zao ipo katika Kiambatisho Na 1.

## *1.3 Ufafanuzi wa maneno*

Kabla ya kuendelea na warsha, maneno muhimu yalifafanuliwa ili kuwaweka washiriki katika upeo mmoja wa kuelewa:

i. **Mtaalamu wa ugani** ni mtu aliyeajiriwa na serikali ili kutoa ushauri wa kitaalamu wa aina mbali mbali kwa jamii ili utumiwe katika maisha ya anayeshauriwa. Wataalamu wa aina hiyo vijijini wanajulikana kama Bwana/Bibi Shamba, Bwana/Bibi Maendeleo, Bwana/Bibi Afya, Bwana/Bibi Mifugo na kadhalika.

ii. **Mkulima/Mfugaji** ni yeyote ambaye maisha yake yanategemea kwa kiasi kikubwa kilimo/ufugaji ikiwa ndiyo sehemu kuu ya shughuli zake za kila siku.

iii. **Mtafiti** ni yeyote ambaye anafanya udadisi wa kisayansi kubaini matatizo au vikwazo vilivyopo katika uendeshaji wa maisha ya mwanadamu na kubuni au kupendekeza utatuzi wake.

iv. **NGO** ni taasisi binafsi isiyo ya kibiashara na haiendeshwi wala kusimamiwa na serikali, yenye lengo la kuwezesha jamii inayolengwa kuwa na mbinu au/na raslimali kwa ajili ya kuboresha hali ya maisha.

v. **Mfanyabiashara** ni yeyote anayejishughulisha na ununuzi wa bidhaa na kuziuza. Mfanyabiashara anaunganisha mzalishaji na mtumiaji kwa madhumuni ya kupata faida. Hata hivyo, mkulima na mfugaji naye anaweza kuwa mfanyabiashara iwapo atazalisha kibiashara yaani kwa madhumuni ya kupata faida kutokana na mtaji atakaowekeza kwenye uzalishaji wake wa mazao au mifugo.

vi. **Kuku wa kienyeji** ni yule aliye wa mbegu ya asili na anatafuta chakula mwenyewe. Baadhi ya washiriki walishauri kuwa hata kuku chotara ambao wanajitafutia chakula wenyewe wanaweza

pia kuwa kuku wa kienyeji. Vile vile sifa zaidi za kuku wa kienyeji ziliainishwa kama ifuatavyo:

- Anafugwa ki-holela - anatafuta chakula mwenyewe
- Hahitaji chakula maalumu ili atage
- Mbegu ya asili (wazawa)
- Anaweza kuatamia na kutunza vifaranga
- Hana rangi maalumu
- Hana umbile maalumu (wana damu mchanganyiko)
- Hutaga mayai kwa kiwango maalumu
- Ladha tofauti ya nyama na mayai ukilinganisha na kuku wa kisasa. Ladha ya kuku wa kienyeji na mayai yake imechangamka kuliko wale wa kisasa.
- Njano ya mayai ya kuku wa kienyeji imekolea na ina ladha nzuri kuliko mayai ya kuku wa kisasa. Rangi ya ute ni nyeupe zaidi kuliko ya mayai ya kuku wa kisasa
- Nyama ya kuku wa kienyeji ni ngumu na inafaa sana kwa kutengeneza supu.

vii. **Soko** ni mabadilishano ya bidhaa (Fedha) kununua / kuuza
viii. **Sokoni** ni mahali maalumu pa kuuziana bidhaa
ix. **Mteja** ni mhitaji anayetaka kununua bidhaa

## *1.4 Matarajio ya washiriki*

Matarajio yaliyoorodheshwa na washiriki yalikuwa kama inavyooneshwa kwenye Kiambatisho Na 6 na kufupishwa kama ifuatavyo:

i. Kuongeza maarifa na ujuzi kuhusu ufugaji bora wa kuku wa kienyeji
ii. Kuweka mkakati wa uboreshaji wa uzalishaji na pato kutokana na kuku wa kienyeji
iii. Kupata ufumbuzi wa matatizo ya kuku hasa magonjwa
iv. Kuelewa matatizo katika utunzaji, magonjwa na uuzaji wa kuku wa kienyeji
v. Kujua namna ya kuboresha kuku wa kienyeji
vi. Kubadilishana uzoefu
vii. Kujua nafasi anayopewa kuku wa kienyeji katika uchumi


### *1.5 Mbinu zilizotumika*

Mbinu mbalimbali za ushirikishwaji zilitumika katika kufanikisha madhumuni ya warsha. Majadiliano yaliendeshwa kwa pamoja na wakati mwingine katika vikundi. Vikundi viligawanywa kwa vigezo vya wakulima/wafugaji kijinsia (wanaume na wanawake peke yao), watafiti, wataalamu wa ugani pamoja na NGO. Kazi zote za vikundi ziliwasilishwa na kujadiliwa kwa pamoja ili kupata makubaliano ya pamoja.

Mbinu mahsusi zilizotumika ni: (i) michoro ya Chapati au Veni. Ukubwa wa miduara ulionesha umuhimu (thamani) wa shughuli inayowakilishwa na duara, umbali wa duara kutoka kitovu cha duara la mzunguko wa maisha ni kiwango cha muda na/au raslimali inayotumiwa katika shughuli inayowakilishwa na duara. (ii) jedwali kufanya mlingano mshazari. (iii) nadharia ya matokeo ya awali ya utafiti juu ya kuku wa kienyeji kutoka kwa mtafiti mmoja wa SUA (Kiambatisho Na. 5).

# 2.0 HALI YA UZALISHAJI WA KUKU WA KIENYEJI

Kuwepo kwa kuku wa kienyeji wengi vijijini na kutopata wanunuzi kila mfugaji anapohitaji kuuza kuku wake inaashiria kutokuwepo kwa soko linaloeleweka la kuku wa kienyeji. Mfugaji hajui



mnunuzi wa kuku wa kienyeji yuko wapi. Mnunuzi pia hana Uhakika wa kuuziwa kuku wa kienyeji na mkulima hata kama kuku wa kienyeji ni wengi kwa vile kuku wa kienyeji hafugwi kibiashara. Mtazamo wa washiriki kuhusu msukumo wa bei katika soko la kuku wa kienyeji unavyooneshwa na kielelezo kifuatacho.

Kielelezo hicho kinaonesha kuwa bei ya kuku wa kienyeji kijijini inasukumwa zaidi na shida ya muuzaji (mfugaji) na wala si msukumo wa kibiashara. Kama mfugaji ana shida huwa tayari kumuuza kuku wake kwa bei yoyote japo kwa shingo upande. Lakini kama hana shida hayupo tayari kumuuza kuku wake labda kwa bei kubwa sana ambayo aghalabu wanunuzi hushindwa. Ilibainika kuwa wafugaji wengi huwatafuta wanunuzi kwa udi na uvumba wanapohisi kuwa kuku wao wameingiliwa na ugonjwa. Wafugaji huuza kuku wagonjwa kwa hila bila kuwafahamisha wanunuzi hali ya kuku wao.

## 2.1 Umuhimu wa kuku wa kienyeji

Kiwango cha jinsi kuku wa kienyeji anavyothaminiwa na kushughulikiwa ikilinganishwa na shughuli zingine. Washiriki waliorodhesha shughuli mbalimbali muhimu wanazojishughulisha nazo katika maisha yao ya kila siku kwa mujibu wa makundi yaliyowakilishwa katika warsha yaani wakulima wanawake, wakulima wanaume, wagani, NGOs, na watafiti kama ilivyooneshwa kwenye Kiambatisho Na. 2.

Maswali mawili waliyojiuliza washiriki ambayo yalikuwa ni changamoto ya majadiliano katika vikundi ni:

i. Je unamthamini kuku wa kienyeji kwa kiasi gani au anachangia kwa kiasi gani kipato katika kaya au mafanikio ya shughuli yako ukilinganisha na shughuli zingine muhimu?
ii. Ni kwa kiasi gani unajishughulisha na kuku wa kienyeji ukilinganisha na shughuli zingine muhimu?

Kila kikundi cha washiriki kilizipanga shughuli zao za kila siku katika mzunguko wa maisha katika mchoro wa 'chapati' kama inavyooneshwa kwenye mchoro Kiambatisho Na. 3a-e. Ukubwa wa

duara unaonesha kiasi cha mchango wa pato au umuhimu wa shughuli. Umbali wa duara kutoka kwenye kitovu cha duara la mzunguko wa maisha unaonesha kiwango cha kujishughulisha na shughuli.

Kwa ujumla matokeo ya michoro ya chapati yalithibitisha kuwa makundi yote yaliyowakilishwa kwenye warsha hayajaona thamani ya kutosha kutokana na kuku wa kienyeji. Japo kwa kiasi fulani wagani na watafiti wanaona kuwa kuku wa kienyeji ana nafasi kubwa ya kuweza kuchangia katika pato la kaya.

Kutokana na matokeo hayo ilionekana kuwa kuku wa kienyeji hathaminiwi na makundi karibu yote yaliyowakilishwa kwenye warsha. Mkulima mwenyewe japokuwa anategemea sana kuku wa kienyeji kwa shida mbalimbali hamfugi kuku huyo kibiashara. Washiriki waliridhika kuwa hali hiyo ndiyo inayopelekea kuku wa kienyeji kutokidhi haja ya soko.

## 2.2 Sababu zinazosababisha kuku wa kienyeji asithaminiwe

Wanawarsha walikubaliana kuwa hali isingekuwa kama ilivyo hivi sasa iwapo upo uwezekano wa hali kuwa njema na yenye neema kutokana na kuku wa kienyeji, iwapo hapangekuwa na sababu zinazopelekea kuwepo hali hiyo. Hivyo wanawarsha walijiuliza kuwa: ni sababu zipi au matatizo yapi yanayochangia kufanya kuku wa kienyeji asithaminiwe kama chanzo muhimu cha mapato ya kaya na uchumi wa taifa? Kila kikundi kiliorodhesha sababu hizo na kuzipatia kipaumbele cha utatuzi.

## 2.2.1 Matatizo na kipaumbele kwa mujibu wa wakulima wanawake

| | MATATIZO | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Ufugaji holela | X | | | | |
| 2. | Magonjwa | 1 | X | | | |
| 3. | Madawa ghali na adimu | 3 | 3 | X | | |
| 4. | Elimu duni | 4 | 4 | 4 | X | |
| 5. | Madawa yanayouzwa yameisha muda | 5 | 5 | 5 | 4 | X |
| | **Uzito wa tatizo** | 1 | 0 | 2 | 4 | 3 |
| | **Kipaumbele** | 4 | 5 | 3 | 1 | 2 |

Ufafanuzi wa matatizo

(1) Ufugaji holela usiojali hali na ustawi wa kuku wa kienyeji. Malazi, malisho na utabibu duni.

(2) Magonjwa kama 'mdondo au kideri' (new castle), ndui ya kuku (chicken pox), kuharisha na kuvimba vichwa.

(3) Madawa ghali na adimu. Madawa mengi yanauzwa kwa vipimo vikubwa vyenye bei kubwa na utumiaji wake unahitaji usafirishaji wa haraka na vifaa maalumu ambavyo ni ghali kuvipata.

(4) Elimu duni ya ufugaji. Kutojua mbinu sahihi na bora za ufugaji wenye tija

(5) Upatikanaji wa wataalamu ni mdogo. Wataalamu wachache na waliopo hawapo tayari kutoa huduma inayostahili.

(6) Utaalamu wa kutengeneza chakula ni mdogo. Hawajui kama upo uwezekano wa kumtengenezea kuku wa kienyeji chakula cha nyongeza kama kile anachotafuta mwenyewe.

(7) Madawa yanayouzwa hayafanyi kazi kwa kuwa yanakuwa yameisha muda (expired) wake na muuzaji anaweza kumdanganya mnunuzi.

(8) Wataalam hawatupatii elimu jinsi ya kutumia madawa.

### 2.2.2 Matatizo na kipaumbele kwa mujibu wa wakulima wanaume

| No | Tatizo | 1 | 2 | 3 | 4 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Elimu duni kuhusu ufugaji bora wa kuku wa kienyeji | X | | | |
| 2. | Magonjwa | 1 | X | | |
| 3. | Urithi wa mfumo wa ufugaji wa kizamani usio na tija | 1 | 2 | X | |
| 4. | Kuku wa kienyeji hawafugwi kibiashara | 2 | 1 | 4 | X |
| | Uzito wa tatizo | 3 | 2 | 0 | 1 |
| | **Kipaumbele** | 1 | 2 | 4 | 3 |

Ufafanuzi wa matatizo

(1) Elimu ndogo ya ufugaji
- Kukosa matunzo mazuri.
- Kukosa ushauri wa kutosha kutoka kwa wataalamu.

(2) Magonjwa ya mulipuko-kama kideri, ambacho kinaweza kikamaliza banda zima kwa muda mfupi.

(3) Urithi wa ufugaji kutoka kwa vizazi vilivyotangulia.
- Kuku wa kienyeji hawafugwi kwa biashara bali kama mboga ya wageni na kwa ajili ya uganga.
- Kuku amefanywa kama matumizi ya vilio, ugeni na sherehe

### 2.2.3 Matatizo na kipaumbele kwa mujibu wa wagani

| Na | Tatizo | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Sera za wizara /NGO's kutothamini umuhimu wa kuku wa kienyeji | X | | | | |
| 2. | Ukosefu wa vitendea kazi na mishahara midogo kwa wagani | 1 | X | | | |
| 3. | Uchache wa wagani kulinganisha na idadi ya wakulima | 1 | 2 | X | | |
| 4. | Elimu duni kwa baadhi ya wagani kuhusiana na fani ya mifugo | 1 | 2 | 3 | X | |
| 5. | Wagani kuwajibika kwa wizara zaidi ya moja | 1 | 2 | 3 | 4 | X |
| | Uzito wa tatizo | 4 | 3 | 2 | 1 | 0 |
| | **Kipaumbele** | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |

Ufafanuzi wa matatizo

1. Wizara husika / NGOs kutothamini umuhimu wa kuku wa kienyeji. Hakuna mkazo wa kisera au mikakati ya kumwendeleza kuku wa kienyeji kama sehemu muhimu ya pato la taifa.

2. Ukosefu wa vitendea kazi, mishahara midogo na maslahi duni kwa wagani kama usafiri, vifaa vya tiba n.k.vinafanya wagani kutotumia ubunifu wao katika kazi.
3. Uchache wa wagani kulinganisha na wakulima unafanya wagani kujali shughuli ambazo ni muhimu zaidi kulingana na matakwa ya wakulima na wafugaji wenyewe.
4. Elimu duni kwa baadhi ya wagani kuhusiana na fani ya mifugo.
5. Wagani kuwajibika kwa wizara zaidi ya moja. Hivi sasa wanawajibika kwa Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Ushirika na Masoko, Wizara ya Maji na Mifugo, Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa.

### 2.2.4 Matatizo na kipaumbele kwa mujibu wa NGOs

| Na | TATIZO | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Wafadhili hawajatoa kipaumbele kwa kuku wa kienyeji | X | | | | | |
| 2. | Jamii haijathamini kuku wa kienyeji | 2 | X | | | | |
| 3. | Mfumo dhaifu wa soko | 3 | 3 | X | | | |
| 4. | Uzalishaji wa kuku wa kienyeji hauna tija | 4 | 2 | 3 | X | | |
| 5. | Sera za ugani Serikalini zinamdhalilisha kuku wa kienyeji | 5 | 2 | 3 | 4 | X | |
| 6. | Mfumo wa elimu unatawaliwa na udhamini wa mambo ya kisasa | 6 | 2 | 3 | 4 | 5 | X |
| | Uzito wa tatizo | 0 | 4 | 5 | 3 | 2 | 1 |
| | Kipaumbele | 6 | 2 | 1 | 3 | 4 | 5 |

Ufafanuzi wa matatizo

(1). NGOs nyingi zinategemea wafadhili na wafadhili wengi hawajatoa kipaumbele kwa kuku wa kienyeji.

(2). Jamii haijathamini kuku wa kienyeji. Anafugwa kama mila na desturi tu. Hivyo hawafanyi juhudi kutafuta na kufuata mbinu bora za ufugaji wa kuku wa kienyeji

(3). Mfumo dhaifu wa soko la kuku wa kienyeji. Aina na tabia za watumiaji wa bidhaa za kuku wa kienyeji hazijulikani kwa wauzaji na wazalishaji. Hakuna mahali maalumu katika ngazi za vijijini ambako muuzaji na mnunuzi wa kuku wa kienyeji wanaweza kukutana kwa urahisi. Hata vigezo vya thamani (bei) ya kuku wa kienyeji au mayai yake haviko bayana.

(4). Uzalishaji wa kuku wa kienyeji hauna tija. Faida yake haithaminiki/haileweki kwa mzalishaji.

(5). Sera za ugani katika serikali zinadhalilisha kuku wa kienyeji. Mara nyingi mafunzo yanayotolewa juu ya uzalishaji bora yanalenga kumfanya mkulima afuge kuku wa kisasa badala ya kuelimisha namna ya kuinua uzalishaji kutumia kuku wa kienyeji.

(6). Mifumo ya elimu inatawaliwa na uthamini wa mambo ya kisasa hivyo kuku wa kienyeji hapewi kipaumbele.

## 2.2.5 Matatizo na kipaumbele kwa mujibu wa watafiti

| Na. | Matatizo | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Sera za kilimo | X | | | | | | |
| 2. | Upungufu wa fedha | 2 | X | | | | | |
| 3. | Upungufu wa wataalamu | 1 | 2 | X | | | | |
| 4. | Upungufu wa vitendea kazi | 4 | 2 | 4 | X | | | |
| 5. | Ushirikiano wa wakulima | 5 | 2 | 3 | 4 | X | | |
| 6. | Miundo mbinu | 6 | 6 | 6 | 6 | 6 | X | |
| 7. | Motisha kidogo | 7 | 7 | 7 | 7 | 7 | 7 | X |
| | Uzito wa tatizo | 1 | 4 | 1 | 3 | 0 | 5 | 6 |
| | Kipaumbele | 5 | 3 | 6 | 4 | 7 | 2 | 1 |

Ufafanuzi wa matatizo

1) Sera za kilimo hazijalenga kuku wa kienyeji.
2) Upungufu wa fedha za kutosha kuendesha shughuli za utafiti hufanya watafiti wajali zaidi utafiti wa wanyama wenye tija kama ng'ombe, mbuzi au nguruwe.
3) Upungufu wa wataalamu katika nyanja za matunzo na magonjwa ya kuku wa kienyeji
4) Ukosefu wa vitendea kazi kama madawa ni adimu na ghali
5) Ushirikiano wa wakulima kwa watafiti ni mdogo. Wakulima wengine wanadai malipo ili washiriki katika utafiti ambao ni wa manufaa kwao wenyewe.
6) Motisha kidogo kwa watafiti na matokeo ya kazi zao. Hakuna utaratibu wa kuenzi wabunifu na wagunduzi waliotoa matokeo nadra (rare) na yenye mchango mkubwa katika jamii.
7) Miundo mbinu hafifu katika maeneo ya vijijini. Sehemu zingine hazifikiki kwa urahisi hasa wakati wa masika.

# 3.0 MAPENDEKEZO YA NAMNA YA KUINUA THAMANI YA KUKU WA KIENYEJI KATIKA KUCHANGIA PATO LA KAYA

Washiriki walianisha visababishi, ufumbuzi, mikakati na wajibu wa wadau katika utekelezaji wa ufumbuzi. Kila kikundi kilitoa mapendekezo yake kwa mujibu wa matatizo waliyobainisha kama ifuatavyo:

## 3.1 Mapendekezo ya wakulima wanaume

| Na. | Tatizo, visababishi na ufumbuzi wake | Wajibu wa wadau katika utekelezaji |
|---|---|---|
| 1. | **Tatizo:** Elimu kuhusu ufugaji bora wa kuku wa kienyeji<br>**Visababishi:** Mwamko mdogo kwa wakulima pamoja na viongozi wa serikali ya kijiji<br>**Ufumbuzi:** Elimu ya ufugaji bora wa kuku wa kienyeji itiliwe mkazo (elimu kwa njia mbalimbali) | **Wakulima:** Wawe na mwamko wa kupata elimu, semina, mikutano, redio, magazeti, n.k<br>**Wagani:** Washiriki kutoa elimu na ushauri kwa wakulima.<br>**Watafiti:** Watathmini elimu itolewayo kwa walengwa<br>**NGOs:** Washirikishe jamii kutoa elimu na ushauri na mikopo ya mitaji.<br>**Serikali:** Ihakikishe na kuona kuwa elimu inatolewa; itoe motisha, vitendea kazi na usimamizi thabiti. |
| 2. | **Tatizo:** Magonjwa ya kuku wa kienyeji<br>**Chanzo:** Kukosa chanjo na ufugaji holela<br>**Ufumbuzi:** Kupata chanjo kwa wakati na kuacha kufuga kiholela | **Wakulima:** Wawe tayari kuchanja kwa wakati na kuacha kufuga kiholela<br>**Wagani:** Washiriki kutoa ushauri wa ufugaji bora wa kuku wa kienyeji na kuhamasisha na kusimamia utoaji wa chanjo.<br>**Watafiti:** Kutafiti magonjwa na madawa yenye nafuu katika utumiaji na upatikanaji; pia kutoa mapendekezo jinsi ya kutumia madawa<br>**NGOs:** Kuhamasisha jamii ione uthamani wa kuku wa kienyeji na kusaidia upatikanaji wa mitaji nafuu.<br>**Serikali:** Serikali ya kijiji isimamie na kuhakikisha wafugaji wanafuata ushauri wa kitaalamu katika kukabili magonjwa na kuweka sheria ndogondogo za ufugaji wa kuku wa kienyeji zinazotilia mkazo kampeni za uchanjaji wa kuku wa kienyeji katika ngazi ya kijiji.<br>Serikali kuu idhibiti upatikanaji na viwango vya |

| | | ubora wa madawa |
|---|---|---|
| **Na.** | **Tatizo, visababishi na ufumbuzi wake** | **Wajibu wa wadau katika utekelezaji** |
| 3. | **Tatizo:** Kurithi mfumo wa ufugaji<br>**Chanzo:** Mila na desturi<br>**Ufumbuzi:** Kurekibisha baadhi ya mila na desturi zilizopitwa na wakati. | **Wakulima:** Kuwa tayari na kuchukua hatua za kubadilika<br>**Wagani:** Wawe karibu na wakulima na wafugaji ili waweze kutoa ushauri sahihi na kamilifu kwa moyo mmoja na kwa ufanisi.<br>**Watafiti:** Watafiti sababu na athari za mila mbalimbali kuhusiana na uzalishaji na kuku wa kienyeji na watoe mapendekezo ya kuboresha<br>**NGOs:** Wawe karibu na wakulima ili wajue namna ya kuwasadia kuongeza uzalishaji wa kuku wa kienyeji<br>**Serikali:** Serikali za vijiji kujiwekea mikakati ya kuondokana na mila ambazo zinazorotesha maendeleo. |
| 4. | **Tatizo:** Kuku hafugwi kibiashara<br>**Chanzo:**Kutothaminiwa kama kuku wa kienyeji anaweza kuleta pato katika kaya<br>**Ufumbuzi:**Kuku afugwe kibiashara na athaminiwe kama vianzo vingine vya mapato | **Wakulima:** Kumthamini kuku wa kienyeji na kumfuga kibiashara kwa:<br>i. Kitaalamu: chakula, malazi na tiba<br>ii. Kutunza kumbukumbu zote za uzalishaji ili kujua kiasi cha faida<br>iii. Kufahamu mahitaji ya soko ili kuzalisha kuku wa kienyeji wanaouzika.<br>iv. Kuwa na lengo maalumu la kipato<br>**Wagani:** Wahamasishe wakulima na kuwapa mafunzo ili waweze kufuga kuku wa kienyeji kibiashara na kutathimini mafanikio<br>**NGOs:** Watoe ushauri na kuwawezesha kupata mitaji<br>**Serikali:** Ngazi zote zihakikishe kuona mkulima anapata mafanikio. |

## 3.2 Mapendekezo ya wakulima wanawake

| **Na.** | **Tatizo, visababishi na ufumbuzi wake** | **Wajibu wa wadau katika utekelezaji** |
|---|---|---|
| 1. | **Tatizo:** Elimu duni kuhusu ufugaji wa kuku wa kienyeji<br>**Chanzo:**Kutoelimishwa<br>**Ufumbuzi:** Wakulima waelimishwe | **Wakulima**<br>• Kuwa tayari kupata semina za mara kwa mara.<br>• Kualika wataalamu kukagua miradi ya wakulima na kutoa utalaamu<br>• Kuitumia elimu itolewayo<br>• Kufuata miongozo itolewayo na wataalam kwa vitendo<br>• Kuwatafuta wataalamu ili kutafuta elimu<br>**Wagani:** Wawe na moyo wa kutembelea wakulima |

| | | |
|---|---|---|
| | | mara nyingi.<br>**Watafiti:** Waboreshe elimu ya wakulima kwa teknolojia rahisi na wawe jirani na wakulima kama wagani<br>**NGOs:** Wawezeshe wakulima kufuga kuku wa kienyeji kitaalamu na kibiashara<br>**Serikali kuu:** Iwape wagani usafiri na vitendea kazi muhimu. Iboreshe mtandao wa mawasiliano ya redio hasa RTD isikike vizuri kila mahali. |
| 2. | Tatizo: Madawa ghali<br>**Visababishi:** Uzalishaji mdogo wa kuku wa kienyeji na usio na tija.<br>**Ufumbuzi:** Kupata mitaji na kuongeza uzalishaji wa kuku wa kienyeji kibiashara | **Wakulima:** Kubadilishana mawazo na utendaji kwa njia ya vikundi. Kuanzisha mifuko ya kusaidiana mitaji. (vyama vya kuweka na kukopa).<br>**Wagani:** Watoe ushauri kwa moyo kwa wakulima juu ya kuanzisha vyama vya kuweka na kukopa na mbinu mbadala za kukabiliana na magonjwa hasa kinga.<br>**Watafiti:** Wachunguze na kupata ufumbuzi wa madawa rahisi yanayoweza kutumika kwa urahisi katika mazingira ya vijijini na wafikishe utaalamu huo kwa wakulima.<br>NGOs: Wawasaidie wakulima kupatamikopo midogo midogo ili kukidhi mahitaji yao<br>**Serikali:** Iwezeshe na kusimamia wagani na watafiti kutekeleza wajibu wao kikamilifu. |
| 3. | Tatizo: Magonjwa<br>Visababishi:<br>• Ufugaji holela<br>• Mazingira machafu<br>• na kutokinga kwa njia ya chanjo.<br>**Ufumbuzi:**<br>Kuwaweka kuku katika mazingira bora na kuwapatia chanjo kwa muda unautakiwa | **Wakulima:** Kujenga tabia ya kutafuta elimu kwa<br>1) kusoma magazeti na vijarida<br>2) kusikiliza redio<br>3) kutembelea wataalamu<br>ili kujua mbinu sahihi na rahisi za kudhibiti magonjwa.<br>Kuweka mazingira bora ya ufugaji.<br>**Wagani:** Washiriki kikamilifu katika kuhamasisha utoaji wa chanjo na mafunzo kwa wakulima.<br>**Watafiti:** Watafiti madawa bora na rahisi kutumika na kupatikana.<br>**NGOs:** Kuhamasisha na kuwezesha wafugaji kufuata kanuni bora za ufugaji<br>**Serikali:** Kudhibiti ubora wa madawa yanayouzwa.<br>Wahakikishe madawa yanayouzwa madukani kama ni sahihi |

## 3.3 Mapendekezo ya wagani

| Na. | Tatizo, visababishi na ufumbuzi wake | Wajibu wa wadau katika utekelezaji |
|---|---|---|
| 1. | **Tatizo:** Sera za Wizara /NGOs kutothamini umuhimu wa kuku wa kienyeji.<br>**Visababishi:** Mtindo wa uundaji wa sera wa kwa mfumo wa toka juu kwenda chini. Bila kushirikisha kikamilifu wadau wote muhimu hasa wakulima na wafugaji:<br>**Ufumbuzi:** Sera zitengenezwe kwa mfumo wa toka chini kwenda juu na ushirikishwaji thabiti wa wadau wote. Hasa wakulima na wafugaji. | **Wakulima**: Kuwa tayari kushiriki na kuchangia katika kutoa kipaumbele cha matatizo yao na namna ya kuyatatua.<br>**Wagani:** Kuhamasisha wakulima na wafugaji katika kushiriki uundaji wa sera zinazowahusu. Kupokea mshindo nyuma wa sera na kuurejesha kwa wakulima na wafugaji.<br>**Watafiti:** Kufanya utafiti wa mambo muhimu ya kuzingatia katika uundaji wa sera na kufanya tathmini ya utekelezaji.<br>**Serikali:** Kutambua kipaumbele cha matatizo ya wakulima kwa kuwashirikisha katika uundaji wa sera. |
| 2. | **Tatizo:** Ukosefu wa vitendea kazi na mishahara midogo.<br>**Visababishi:**<br>• Serikali kuu kutegemea zaidi wafadhili kutoa vitendea kazi mfano: IFAD, NAEP n.k<br>• Serikali kuu kutopandisha watumishi wake vyeo kama stahili.<br>**Ufumbuzi:**<br>• Kuacha utegemezi wa wafadhili wa nje katika matumizi muhimu ya serikali.<br>• Kuboresha mfumo wa utumishi na kujali maslahi ya watumishi. | **Wakulima:** Kuongeza uzalishaji na kukuza pato la taifa ili serikali iwe na uwezo wa kumudu gharama za utawala na uendeshaji.<br>**Wagani:**<br>• Wawe na vyama madhubuti vya kutetea na kufuatilia maslahi yao.<br>• Waombe na wawe tayari kukopa vyombo vya usafiri na kuvitumia kwa uangalifu.<br>**NGOs:** Wahusike katika uhamasishaji na uwezeshaji wa harakati za ushawishi na utetezi wa maslahi ya watumishi.<br>**Serikali kuu**:<br>• Ianzishe utaratibu maalumu na unaojitegemea wa kutoa vitendea kazi kwa watumishi wake ikiwa ni pamoja na kutoa mikopo nafuu ya vitendea kazi kama ilivyoanza kwa baadhi ya sekta.<br>• Iboreshe mfumo wa utumishi unaojali waajiriwa kupata stahili zao kadri inavyo bidi. |

| | | |
|---|---|---|
| 3. | **Tatizo:** Uchache wa wagani kulinganisha na idadi ya wakulima<br>**Visababisho:**<br>• Kustaafu<br>• Kuustaafishwa<br>• Vifo hasa vinavyotokana na UKIMWI<br>• Uanzishwaji wa mikoa wilaya, tarafa, kata na vijiji vipya bila kujali uwezo wa serikali.<br>• Wagani kuacha kazi bila taarifa<br>**Ufumbuzi:**<br>• Kutoa ajira mpya kujaza nafasi zilizoachwa wazi<br>• Kuepuka vifo vinavyoepukika<br>• Kuboresha mazingira ya kazi<br>• Kushirikisha wakulima wajuzi katika ugani | **Wakulima:** Kuwa tayari kushirikiana na wenzao ujuzi walionao.<br>**Wagani:**<br>• Wahamasishe wakulima wenye ujuzi wawafundishe wenzao.<br>• Waepuke tabia zinazochangia katika maambukizi ya UKIMWI<br>• Wajenge tabia ya kujiendeleza kielimu<br><br>**Watafiti:**<br>Washiriki kikamilifu kufikisha taaluma walizozibuni kwa walengwa ili zitumike. Wasaidiane na wagani katika jukumu hilo.<br>**NGOs:**<br>Wasaidie kuzalisha wataalamu (hasa wakulima weneyewe) na kuwawezesha kutoa utaalamu huo kwa walengwa.<br>**Serikali:**<br>• Iboreshe mazingira ya kazi na kipimo kiwe ni kupungua kwa idadi ya watumishi wanaoacha kazi, ongezeko la morali ya kazi kwa kuona jinsi watumishi wanavyojituma na kuwa wabunifu katika utendaji wa kazi.<br>• Kuwa na kumbukumbu sahihi ya watumishi wakati wote na kutoa ajira kwa nafasi zinazoachwa wazi.<br>• Serikali kutoa nafasi za mafunzo kwa wagani<br>• Serikali kuu ifanye uchambuzi yakinifu kabla ya kuanzisha maeneo mapya |
| 4. | **Tatizo:** Wagani kuwajibika kwa wizara zaidi ya moja.<br>**Visababishi:**<br>Mabadiliko ya mara kwa mara ya wizara bila kujali ufanisi katika utendaji ngazi za chini.<br>**Ufumbuzi:**<br>Wizara zipangwe kujali ufanisi wa watendaji wa ngazi zote. | **Serikali kuu**<br>Iangalie upya wizara zenye utata wa aina hii hasa kilimo, mifugo na masoko na kuzipanga tena kuzingatia utendaji wa ngazi chini. |

## 3.4 Mapendekezo ya NGOs

| Na. | Tatizo, visababishi na ufumbuzi wake | Wajibu wa wadau katika utekelezaji |
|---|---|---|
| 1. | **Tatizo:** Mfumo dhaifu wa soko.<br>**Visababishi:**<br>• Mkulima hafugi kibiashara hivyo hajui thamani halisi ya kuku /mayai<br>• Hakuna sehemu maalum ya kuuziana bidhaa (kuku)<br>• Hakuna udhibiti wa ubora wa bidhaa na bei ya kuku.<br>• Mnunuzi na mfugaji hawana sehemu maalum ya kukutana.<br>• Mzalishaji na mteja hawana mawasiliano ya kujua bidhaa inayohitajika ina sifa za aina gani<br>• Jamii haithamini kuku wa kienyeji<br>• Kuku wa kienyeji hawachangii vya kutosha uchumi katika pato la kaya.<br>• Mila na desturi zilizopitwa na wakati zinazodumaza kuku wa kienyeji.<br>**Ufumbuzi:**<br>• Kuku wa kienyeji afugwe kibiashara kwa Kuongeza thamani ya kuku wa kienyeji ili awe na mchango wa kutosha katika pato la kaya<br>• Kuwepo na minada ya kata ya kuku wa kienyeji ambapo kutakuwa na udhibiti wa ubora wa kuku na kuwa na utaratibu mzuri wa biashara (vigezo vya bei) | **Wakulima:**<br>• Wafuge kiutaalamu ili waongeze tija kwa kutumia mbinu bora na kutunza kumbukumbu za uzalishaji ili waweze kujua faida wanayopata<br>• Waanzishe ushirika wa kuuza kuku utakaohakikisha na udhibiti wa ubora bidhaa za kuku wa kienyeji na bei pia kuwezesha wanunuzi kufikia soko kwa urahisi na kujua mahitaji ya soko.<br>**Wagani:**<br>• Wahamasishe ufugaji wa kibiashara<br>• Watoe mafunzo ya ufugaji bora<br>• Wazalishe wakulima wakufunzi watakaoshirikiana nao katika uhamasishaji na mafunzo<br>• Washirikiane na wakulima kudhibiti ubora wa bidhaa za kuku wa kienyeji na kutafuta taarifa za masoko.<br>**Watafiti:**<br>• Watafiti mbinu rahisi na zinazotekelezeka ili kuongeza uzalishaji<br>• Wahakikishe matokeo yanawafikia walengwa<br>• Watafiti soko la kuku wa kienyeji. Matakwa ya walaji, namna ya kuwafikia, makadirio ya bei muafaka (optimum prices) kwa kila eneo na ngazi ya mauzo na kama bei zina msimu<br>NGOs:<br>• Wahamasishe ufugaji wa kibiashara<br>• Watoe mafunzo ya ufugaji bora<br>• Uhamasishaji wa uanzishaji wa ushirika na minada<br>• Wawafahamishe wafadhili kuhusu umuhimu wa kuku wa kienyeji<br>• Watafute na kutoa taarifa za masoko.<br>• Wawezeshe upatikanaji wa mikopo na mitaji.<br>**Serikali:**<br>• Wizara ya mifugo/kilimo itilie mkazo katika kuku kienyeji.<br>• Kutilia mkazo uhamiasishaji wa uanzishaji wa ushirika na minada ya bidhaa za kuku wa kienyeji<br>• Serikali za mitaa (ngazi ya kata-wilaya) |

| | | |
|---|---|---|
| | | zisimamie na kuwezesha uanzishaji wa ushirika, vituo vya masoko na uhamasishaji wa utafiti. |
| 2. | **Tatizo:**<br>Mifumo ya elimu inayodhalilisha kuku wa kienyeji.<br>**Visababishi:**<br>• Kasumba ya kuthamini vitu vya kigeni na kuona kwamba vya asili ni duni<br>**Ufumbuzi:**<br>Kutambua sifa bora za kuku wa kienyeji na kuzitumia. | **Wakulima:**<br>• Kushirikiana na watafiti na wagani kuainisha na kutambua kuku wa kienyeji wenye sifa bora za kiuzalishaji.<br>**Wagani:**<br>• Washiriki katika kueneza ufahamu wa ubora wa kuku wa kienyeji na namna ya kutumia ubora huo katika uzalishaji.<br>**Watafiti:**<br>• Waratibu sifa zote za kuku wa kienyeji na namna ya kuzitumia katika kuongeza uzalishaji wake pia washirikiane na wakulima na wagani katika kuhamasisha matumizi ya ubora wa kuku wa kienyeji.<br>**NGOs:** Watangaze na wahamasishe watu kuhusu sifa bora za kuku wa kienyeji<br>**Serikali:** Isimamie na iwezeshe utekelezaji wake. |

## 3.5 Mapendekezo ya watafiti

| Na. | Tatizo, visababishi na ufumbuzi wake | Wajibu wa wadau katika utekelezaji |
|---|---|---|
| 1. | **Tatizo:** Motisha mdogo kwa watafiti unaofanya wasiwe wabunifu na watundu kiasi cha kutosha.<br>**Visababishi:**<br>• Serikali kutojali maslahi ya wataalamu wake kikamilifu<br>• Ushirikiano mdogo wa wakulima na wagani katika utafiti. | **Wakulima na wagani**<br>• Kuwa na ushirikiano na wataalamu katika utafiti hasa unaofanyika katika maeneo ya uzalishaji.<br>**Watafiti:**<br>• Utafiti wanaofanya na wakulima uwe ni ule ulioidhinishwa kuwa una uhakika wa kutoa matokeo mazuri na hauna madhara kwa watumiaji. Watafiti wawe wazi kwa wakulima na wagani juu ya taratibu zote za utafiti.<br>• Matokeo ya utafiti yaratibiwe na yasambazwe sehemu zote hususan kwa watumiaji wa matokeo hayo.<br>**Serikali:**<br>• Iboreshe maslahi ya wataalamu ili wawe na uhakika wa kukidhi mahitaji yao muhimu na matarajio yao ya maisha.<br>• Ianzishe utaratibu wa kuwaenzi watafiti |
| 2. | **Tatizo:** Miundo mbinu duni hasa barabara za vijijini<br>**Visababishi:**<br>• Matengenezo hafifu na | **Wakulima:** Kushiriki kama vikundi katika uboreshaji wa miundo mbinu wakijua kuwa ni kwa manufaa yao wenyewe.<br>**Wagani:** Wahamasishe wakulima juu ya |

| | | |
|---|---|---|
| | ya nadra kwa barabara za vijijini.<br>• Ushiriki mdogo wa wananchi katika kuchangia uboreshaji wa miundo mbinu vijijini. | umuhimu wa kushiriki katika kuimarisha miundo mbinu.<br>**NGOs:**<br>• Wawezeshe upatikanaji wa wafadhili kwa jamii kwa ajili ya uboreshaji wa miundo mbinu.<br>• Washirikiane na wananchi katika utunzaji na uboreshaji wa miundo mbinu<br>**Serikali:**<br>• Itenge fedha kwa makusudi ya kuboresha miundo mbinu ya vijijini.<br>• Serikali za Wilaya kuhakikisha kuwa sehemu kubwa ya mapato ya vijiji inarudishwa vijijini kwa ajili ya kuboresha miundo mbinu. |
| 3 | **Tatizo:**<br>• Upungufu wa vitendea kazi<br>• Fedha kidogo kununua vifaa na madawa<br>**Visababishi:** Mgawo mdogo wa fedha toka serikalini kwa ajili ya utafiti<br>**Ufumbuzi:**<br>Kuongeza fedha za utafiti na ufanisi katika utendaji na matumizi | **Wakulima:** Kuchangia gharama za utafiti kwa hali na mali pale ambapo utafiti unafanyika katika mazingira ya uzalishaji.<br>**Wagani:** Wahamasishe wakulima katika kuchangia utafiti.<br>**Watafiti:** Watumie kwa ufanisi fedha na raslimali zilizopo. Utunzaji na ubunifu wa vitendea kazi<br>**Serikali:**<br>Iongeze bajeti ya utafiti kwa kiwango cha kutosheleza mahitaji ya utafiti. |
| 4. | **Tatizo:**<br>Sera za kilimo haziweki bayana nafasi ya kuku wa kienyeji katika pato na uchumi wa taifa.<br>**Visababishi:**<br>• Kutothaminiwa kuku wa kienyeji<br>• Kutoshirikisha walengwa kutayarisha sera<br>• Mapato na umuhimu wa kuku wa kienyeji katika kaya na taifa hauko bayana.<br>**Ufumbuzi:**<br>Sera ya kilimo/ufugaji iweke bayana umuhimu wa kuku wa kienyeji katika pato la kaya na taifa na mikakati ya kuinua uzalishaji wake. | **Wakulima:**<br>• Washiriki katika uundaji wa sera na waonyeshe umuhimu wa kuku wa kienyeji kwa vitendo katika uzalishaji.<br>**Wagani:**<br>• Waelimishe wakulima juu ya sera za kilimo, wajibu na umuhimu wao katika kushiriki kwenye utayarishaji wa sera<br>**Watafiti:**<br>Wazijue sera na kutoa mapendekezo ya marekebisho<br>Mipango ilenge sera zilizopo<br>**Serikali**<br>Ihakikishe kuwa sera kuhusu kuku wa kienyeji inatayarishwa kwa uzito wa kutosha kuwezesha kuinua uzalishaji wa kuku wa kienyeji. |

| | | |
|---|---|---|
| 5. | **Tatizo:**<br>Upungufu wa wataalamu katika nyanja ya kuku wa kienyeji.<br>**Visababishi:**<br>• Mitaala kutotilia mkazo kuku wa kienyeji<br>• Ajira kuwa ngumu serikalini<br>• Posho ndogo<br>**Ufumbuzi:**<br>• Mitaala izingatie kuku wa kienyeji<br>• Ajira za wataalamu zipewe kipaumbele<br>• Posho ziboreshwe<br>• Wataalamu kupewa mafunzo rejea<br>• Wakulima wa mifano wawepo | **Wakulima:**<br>Wakulima wenye ujuzi kusaidia wenzao katika kubaini na kutatua matatizo katika uzalishaji.<br>**Watafiti:**<br>Wasaidie kuandaa mitaala itakayoinua kiwango cha kuku wa kienyeji katika mafunzo ya wataalamu<br>**Serikali na NGOs**<br>Kutoa nafasi zaidi ya mafunzo na ajira kwa wataalamu hasa katika nyanja ya kuku wa kienyeji. |

# 4.0 MAAZIMIO YA WARSHA

Washiriki waliazimia kuwa kila mmoja wa washiriki atakapo rejea kwake aanze kutekeleza yale ambayo anaweza kuyatekeleza kwa uwezo wake mwenyewe. Hivyo kila mshiriki aliandika katika kadi kile/yale ambayo anatarajia kwenda kuyafanya mara tu atakaporejea kwake. Mradi wa TARP II SUA uliahidi kufuatilia kila mshiriki ili kuona jinsi anavyotekeleza aliyoahidi na kuratibu matokeo. Ahadi za utekelezaji walizotoa washiriki zimeorodheshwa katika Kiambatisho Na. 4.

# 5.0 TATHMINI YA WARSHA

Washiriki walifanya tathmini ya mwenendo wa warsha kwa kulinganisha na:

i. Matarajio waliyokuwa nayo kuhusu ushiriki wao katika warsha
ii. Jinsi uendeshaji wa warsha ulivyokidhi madhumuni ya mada

Kila mshiriki aliandika kwa siri tathmini yake kwenye kadi bila kuandika jina lake. Matokeo ya tathmini hiyo yameoneshwa kwenye jedwali lifuatalo.

| SWALI | Idadi ya waliojibu | | |
|---|---|---|---|
| | **Sana** | **Wastani** | **Hapana** |
| Je warsha imekidhi matarajio yako? | 18 | 9 | 0 |
| Je mwenendo wa warsha umewezesha kufikia madhumuni ya mada? | 20 | 7 | 0 |

# 6.0 KUFUNGA WARSHA

Warsha ilifungwa rasmi na Profesa A.J.P. Tarimo kwa kuwaasa washiriki kuwa mfano wa kuigwa katika utekelezaji wa maazimio ya warsha. Baada ya kuwatakia safari njema ya kurudi makwao Profesa Tarimo aliifunga rasmi warsha mnamo saa 11.30 jioni tarehe 4 Desemba 2002.

# 8. VIAMBATISHO

## Kiambatisho Namba 1: Orodha kamili ya washiriki wa warsha

| Na | Jina | Jinsia | Kazi | Kijiji / Taasisi | Kata / Tarafa | Anuani |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Anjelina J. Ngonyani | Ke | Mkulima | Litapwasi | Mtipindi | SLP 2 Peramiho |
| 2 | Bernadetha A Mbare | Ke | Mkulima | Kbaoni | Chokaa | SLP 107 Chunya |
| 3 | Happy Mkupasi | Ke | Mkulima | Katenge | Wanging'ombe | SLP 1129 Njombe |
| 4 | Joyce M Nyembele | Ke | Mkulima | Isongole | Isongole | SLP 160 Ileje |
| 5 | Judi Mwampashi | Ke | Mkulima | Mponela | Mbozi Sanduka | SLP 303 Mbozi |
| 6 | Karolina Chaula | Ke | Mkulima | Katonto | | SLP 229 Sumbawanga |
| 7 | Leokadia O Nyalusi | Ke | Mkulima | Lulanzi | Kilolo | SLP 647 Iringa |
| 8 | Osmunda A Ndonde | Ke | Mkulima | Matalawe | | SLP 366 Songea |
| 9 | Paskazia Samsoni | Ke | Mkulima | Kaukwale | Senga | SLP 232 Sumbawanga |
| 10 | Bickson Mbughi | Me | Mkulima | Mponela | Mbozi Sanduka | SLP 303 Mbozi |
| 11 | Chale M Msagamila | Me | Mkulima | Uyahudini | Mtipindi | SLP 221Peramiho |
| 12 | Donald Kahenga | Me | Mkulima | Igundu | Kahua | SLP 33 Chunya |
| 13 | Fidelis K Palamiho | Me | Mkulima | Katenge | Wanging'ombe | SLP 1129 Njombe |
| 14 | John Mwatwambo | Me | Mkulima | Itumba | Itumba | SLP 45 Ileje |
| 15 | Onesmo J Mgumba | Me | Mkulima | Lupalama | Ulanda | SLP 46 Tosamaganga |
| 16 | Titus Namwala | Me | Mkulima | Kaengesa | Kaengesa | SLP 229 Sumbawanga |
| 17 | Zenobi M Mwanakatwe | Me | Mkulima | Kanondo | Ntendo | SLP187 Sumbawanga |
| 18 | Alice J Mwang'amba | Ke | Mgani | Mponela | Mbozi Sanduka | SLP 94 Mbozi |


| Na | Jina | Jinsia | Kazi | Kijiji / Taasisi | Kata / Tarafa | Anuani |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 19 | Gustavol C Mgoda | Me | Mgani | Katenge | Wanging'ombe | SLP 168 Njombe |
| 20 | Japhet M Mbonile | Me | Mgani | | | SLP 232 Sumbawanga |
| 21 | Sammy F Moshi | Me | Mgani | | | SLP 174 Songea |
| 22 | Gelda H Mpunda | Ke | NGO | CDTF (Community Development Trust Fund) | | SLP 779 Songea |
| 23 | Luiza F Almasi | Ke | NGO | ADP Isangati Trust Fund | | SLP 1687 Mbeya / SLP 1241- MIICO Mbeya |
| 24 | Simon H Mwang'onda | Me | NGO | Ileje Rural Development Trust Fund | | SLP 160 Itumba-Ileje /SLP 1241 MIICO. Mbeya |
| 25 | Jackson K Murro | Me | Mtafiti | ARI-Uyole | | SLP 400 Mbeya |
| 26 | Elikunda C Kimbi | Me | Mtafiti | ARI-Uyole | | SLP 400 Mbeya |
| 27 | Kenyela SA Mgawe | Me | Mtafiti | ARI-Uyole | | SLP 400 Mbeya |
| 28 | Rogers E Malimbwi | Me | Mtafiti | SUA | Morogoro | SLP 3013 Morogoro |
| 29 | Amandus Muhairwa | Me | Mtafiti | SUA | Morogoro | SLP 3021, SUA, Morogoro |
| 30 | Fulgence Mishili | Me | Mtafiti | SUA | Morogoro | SLP 3007 SUA Morogoro |
| 31 | Emmanuel Batamuzi | Me | Mtafiti | SUA | Morogoro | SLP 3020 Morogoro |
| 32 | Joyce Lyimo-Macha | Ke | Mtafiti | SUA | Morogoro | SLP 3044 Morogoro |
| 33 | Akwilin JP Tarimo | Me | Mtafiti | SUA | Morogoro | SLP 3035 Morogoro Simu 0744 477790 |
| 34 | Amin Bakari | Me | Mwezeshaji | INTERMON OXFAM | Morogoro | S LP 3236 Morogoro Simu: 023 3228, 0744626706 |
| 35 | Elimpaa Kiranga | Me | Ofisa Kiungo (Utafiti-Ushauri) | ARI-Uyole | | SLP 400 Mbeya |

## Kiambatisho Namba 2: Shughuli muhimu ambazo washiriki wanajishughulisha nazo katika maisha yao ya kila siku

| | |
|---|---|
| **a. Wakulima wanawake**<br>1. Kilimo<br>2. Ufugaji wa kuku wa kienyeji<br>3. Kazi za nyumbani<br>4. Ufugaji wa kuku wa kisasa<br>5. Biashara ndogondogo | **b. Wakulima wanaume**<br>1. Kilimo<br>2. Ufugaji ngo'mbe<br>3. Ufugaji wa mbuzi na kondoo<br>4. Ufugaji sadifu<br>5. Biashara<br>6. Ufugaji kuku wa kienyeji |
| c. Wagani<br>1. Tiba/kinga kuku wa kienyeji<br>2. Tiba/kinga ngo'mbe<br>3. Taarifa za kila mwezi<br>4. Mikutano ya kitaalam na utafiti<br>5. Ushauri mazao<br>6. Tiba wanyama wadogowadogo<br>7. Ushuru mazao ya mifugo<br>8. Mikutano na warsha<br><br>**d. Watafiti wa mifugo wanajishughulisha na**<br>1. Utafiti wa kuku mzawa<br>2. Utafiti wa masoko<br>3. Utafiti wa kuku wa kisasa<br>4. Utafiti wa ng'ombe maziwa<br>5. Kutoa mafunzo wataalamu na wakulima<br>6. Kutoa ushauri kwa wakulima na wafugaji<br>7. Utafiti wa nguruwe<br>8. Kuandaa na kutoa taarifa na majarida juu ya matokeo ya utafiti | e. NGO<br>1. Ushauri na mafunzo<br>i. Mazao ya chakula<br>ii. Mazao ya biashara<br>iii. Ufugaji wa ng'ombe<br>iv. Ufugaji wa mbuzi/nguruwe<br>v. Ufugaji wa kuku wa kisasa<br>vi. Ufugaji wa kuku wa kienyeji<br>vii. Mazingira<br>2. Huduma za jamii<br>3. Utunzaji na uhifadhi wa mazingira<br>4. Ushawishi na utetezi<br>5. Akiba na mikopo<br>i. Biashara<br>ii. Ufugaji - ng'ombe<br>iii. Ufugaji - mbuzi/nguruwe<br>iv. Kuku wa kisasa<br>v. Kuku wa kienyeji<br>6. Misaada ya kibinadamu kwa wahanga mbalimbali. |

## Kiambatisho Namba 3: Michoro ya chapati (veni) kuonesha shughuli na washiriki wa warsha wanavyojishughulisha nazo.


### 3a. Mchoro wa chapati (veni) kikundi cha wakulima wanaume




*Kielelezo cha namba za miduara*

1. Kilimo
2. Ufugaji ng'ombe
3. Ufugaji wa mbuzi na kondoo
4. Ufugaji sadifu
5. Biashara
6. Ufugaji kuku wa kienyeji


## 3b. Mchoro wa chapati (veni) kikundi cha wakulima wanawake





*Kielelezo cha namba za miduara*

1. Kilimo
2. Ufugaji wa kuku wa kienyeji
3. Kazi za nyumbani
4. Ufugaji wa kuku wa kisasa
5. Biashara ndogondogo

## 3c. Mchoro wa chapati (veni) kikundi cha wagani




## 3d. Kielelezo cha chapatti (veni) kikundi cha NGOs.




**Kielelezo cha namba za maduara**

1. Ushauri na mafunzo
2. Huduma za jamii
3. Utunzaji na uhifadhi wa mazingira
4. Ushawishi na utetezi
5. Akiba na mikopo
    i. Biashara
    ii. Ufugaji - ng'ombe
    iii. Ufugaji - mbuzi/nguruwe
    iv. Kuku wa kisasa
    v. Kuku wa kienyeji
6. Misaada ya kibinadamu kwa wahanga mbalimbali.

## 3e. Mchoro wa chapati (veni) kikundi cha Watafiti



## Kiambatisho Na 4: Ahadi za utekelezaji wa maazimio ya warsha

**BICKSON MBUNGI**
Mambo nitakayofanya baada ya kufika nyumbani
(1) Nitawashauri wana kikundi wenzangu juu ya kuimarisha mabanda ya kuku.
(2) Nitawajulisha wenzangu wafugaji wa kuku, kutunza kumbukumbu za ufugaji
(3) Nitawakumbusha wanakikundi kufungua akaunti Benki

**GELDA MAPUNDA**
(1) Kama NGO nina vikundi ambavyo tunashirikiana nao nitaanza kuwahamasisha kuhusu kuku wa kienyeji.
(2) Nitatoa pia elimu kwa vikundi hivyo .
(3) Kwa kuanzia ili niwaeleze watu kitu kilicho hai nitaanza kufuga kuku wa kienyeji badala ya kuku wa kisasa.

*FIDELIS. K. PELAMIHO*
(1) Kutoa maelezo kuhusu semina niliyopata.
(2) Kushirikiana nao kufuga kuku wa kienyeji
(3) Kuomba uongozi wa kijiji kusimamia na kutambua kuwa mkulima anafuga kuku
(4) Kuwaelimisha wafugaji kuhusu ufugaji wa kuku wa kienyeji

**TITUS NAMNALA**
Mambo muhimu nitakayofanya nitakaporudi;
(1) Kwanza nitazingatia sana ufugaji wa kuku wa kienyeji ili kuinua pato langu.
(2) Nitawaelimisha wenzangu mfumo mpya wa kuku wa kienyeji

**HAPPY MKUPASY**
(1) Nitakwenda kuwapatia wenzangu kile nilichokuja kukichukuwa au yale niliyojifunza
(2) Ili na wenzangu wajisikie kweli ni cha muhimu

**PASKALIA SAMSONI**

(1) Mimi nikifika nitawaelimisha wale wasio kwenye kikundi wajiunge na kikundi.
(2) Nakuwaeleza kuku wa kienyeji akithaminiwa anaweza akatuondolea umaskini
(3) Wakikubali katika kuingia kwenya vikundi natawaeleza juu ya chanjo.

**BERNADETHA A. MBARE**

Nikifika chunya nitafanya mambo yafuatayo.

(1) Nitaanza kufuga kuku wa kienyeji.
(2) Nitawasimulia wenzangu yote tuliofundishwa
(3) Nitajitahidi mimi mwenyewe ili waone mfano mzuri na inategemea wanaweza wakatamani
(4) Nitawasisitiza waganga ili waweze kuhamasisha wakulima kuhusu ufugaji wa kuku wa kienyeji.
(5) Nitawaeleza jinsi ya kutumia dawa ya kideri ambayo ndio kero kubwa katika kijiji chetu.

**CHALE M. MSAGAMILA**

(1) Kuanzisha ufugaji wa kuku wa kienyeji katika mfumo wa kibiashara
(2) Kuhamasisha wanakijiji wenzangu nao kuanza kuthamini kuku wa kienyeji na kuwafuga kwa lengo la biashara ili kuongeza kipato katika kaya
(3) Nitahamasisha ushirikiano wa wafugaji kuanzia kaya moja hadi nyingine ili kuweza kutafuta matatizo yanayohitaji gharama kubwa ya fedha kwa pamoja.

**DONALD KAHEMA**

(1) Nikirudi nyumbani nitajitahidi kuwaelimisha wanakijiji wenzangu umuhimu wa kufuga kuku wa kieyeji kwa juhudi na kuwajulisha kuwa umefikia wakati sasa kuona kuwa kuku wa kienyeji wakitunzwa vizuri wanaweza kutumia kupata kipato.

**ANGELINA J. NGONYANI**

(1) Kujenga kibanda safi cha kuku.
(2) Nitakiitisha kikao kueleza jinsi ya mipango mizuri ya ufugaji wa kuku wa kienyeji
(3) Nakuanza kupanga vikundi ili kusiwe na matatizo kama kuchanja chanjo na hasa mimi mwenyewe niwe ni mfano.

**JUDI MWAMPASHI**

(1) Nitamuomba mtendaji aniitie wananchi wote katika huo mkutano wa hadhara nitawaelimisha wananchi yote ambayo nimefundishwa.

**LEOKIDA OSICA NYALUSI**

(1) Nitakwenda kuelimisha juu ya ufugaji kuku wa kienyeji
(2) Nitakwenda kuboresha vikundi ili tupate maendeleo
(3) Nitasisitiza sana juu ya kuboresha kuku wa kienyeji

**ONESMO JOHN MGUMBA**

Kutokana na haya niliyojifunza mambo muhimu nitakayokwenda kufanya :

(1) Kutayarisha mahali au sehemu ya kuanza kufuga au kufugia kuku wa kienyeji vizuri zaidi ya awali.
(2) Kuwapa elimu kama familia yangu
(3) Halafu kuelimisha majirani

**ZENOBI MWANAKATISE**

Nikirudi nyumbani nitafanya yafuatayo:

(1) Nitaenda kuendeleza ufugaji wa kuku ambao ninao
(2) Nitakwenda kuwapelekea wanakikundi ujumbe niliotoka nao hapa kwenye warsha

**SIMON H. MWANGONDA**

(1) Kuwatembelea wafugaji katika eneo la kazi ya taasisi na kupata takwimu za ufugaji kuku wa kienyeji na hali ya soko
(2) Kutoa taarifa ya warsha - mrejesho wake -ambao utakuwa umeandikwa na kutafakari namna ya kufanya kazi. Ili kufanikiwa tunaomba wawezeshaji watoe mrejesho mapema

ambao utakuwa umeandikwa mambo yote muhimu yaliyojadiliwa kwenye warsha

**JOHN MWATWAMBO**

(1) Kuboresha banda la kuku na sehemu ya vifaranga
(2) Nitawahamasisha majirani zangu kuthamini kuku wa kienyeji
(3) Kutoa chanjo kuzuia kideri pamoja na jirani zangu.

**JACKSON K. MURRO**

(1) Kuendelea na utafiti wetu juu ya kuku wa kienyeji na kurekebisha mwelekeo ili kumnufaisha mkulima zaidi
(2) Kuwasaidia wakulima katika vikundi vyao namna ya kuweza kupata minada zaidi endapo watakwama au watapiga hatua zaidi ( kuimarisha vikundi vya ufugaji kuku vya wakulima)

**KENYELA MGAWE**

Nikitoka hapa nitafanya au kuendeleza yafuatayo

(1) Kuendeleza shughuli za utafiti wa kuku wa kienyeji kwa ari zaidi.
(2) Kuendeleza utoaji wa ushauri kwa wakulima kuhusiana na kuku wa kienyeji kama chanzo rahisi cha pato la kaya na njia rahisi ya kujipatia lishe bora

**LUIZA F. ALMASI**

(1) Kuhamasisha ufugaji wa kuku wa kienyeji kibiashara
(2) Kutoa mafunzo ya ufugaji bora wa kuku wa kienyeji

**AMIN BAKARI**

(1). Nitashauri mashirika yasiyo ya kiserikali ninayofanya nayo kazi kuanzisha vikundi/ushirika na wakulima wa kufuga na kuuza kuku wa kienyeji.

**AMANDUS MUHAIRWA**

(1) Kutoa maandiko juu ya nyumba bora za kuku wa kienyeji kwa matumizi ya wakulima
(2) Kuendelea na utafiti wa kuku wa kienyeji

**OSHUDA NDONDE**

(1) Kukutana na wanakikundi wenzangu na kuwapa elimu niliyoipata

(2) Kuwahimiza wanakikundi waanze mara moja ufugaji wa kuku wa kienyeji

(3) Nitashirikiana na wanakikundi kutafuta soko la uhakika

**FULGENCE MISHILI**

(1) Kuandaa mikakati ya kutoa vipeperushi kuhusu masoko ya kuku wa kienyeji

(2) Kuhamasisha watu / jamii inayonizunguka juu ya umuhimu wa kuku wa kienyeji

**KAROLINA CHAULA**

(1) Nitaboresha mradi wangu wa kuku wa kienyeji

(3) Nitawashawishi wenzangu ili tuungane pamoja tuunde kikundi chetu cha wafugaji wa kuku wa kienyeji

**SAMMY MOSHI**

(1) Kutoa taarifa kwa DEO- Songa kumpa maagizo ya warsha ili utekelezaji wa kuanza kumjali kuku wa kienyeji uanze mara moja

(2) Nitaanza kufuga kuku kiasi ili kuwa mfano kwa wagani /wakulima

(3) Wakulima walio wakilisha watakuwa chachu kwa kuanza elimu hiyo kwa wenzao.

**GUSTAJOL C. MGODA**

(1). Kufanya mikutano na kuwaelimisha wakulima juu ya:

- Nafasi ya kuku wa kienyeji katika kuchangia pato la mkulima
- Umuhimu wa chanjo za kuku na upatikanaji wake
- Namna ya kuboresha mifumo ya ufugaji kuku wa kienyeji

**JAPHET MBONILE**

(1) Kuwashauri wafugaji juu ya ujenzi wa mabanda ya kufugia kuku wa kienyeji.
(2) Kuwaelimisha wafugaji juu ya kuzingatia muda wa chanjo kila baada ya miezi mitatu
(3) Kuwaelimisha wafugaji juu ya umuhimu wa kuku wa kienyeji kiuchumi

**JOYCE MSUKWA NYEMBELE**

(1) Nitawaita wanakikundi wenzangu na kuwaelimisha niliyojifunza
(2) Wakisha elimishwa ndipo tutakapoanza mikakati mizuri zaidi ya ufugaji bora kuliko mwanzoni.

## Kiambatisho Namba 5: Ushauri wa kitafiti juu ya kuku wa kienyeji

Hatua muhimu za ufugaji bora wa kuku wa kienyeji

- Kuwa na nia ya kufuga kuku wa kienyeji
- Tayarisha malazi ya kuku (mfano banda la gharama nafuu)
- Pata kuku majike
- Tengeneza mahali pakutagia (sehemu iliyojificha kidogo kama kwenye boksi)
- Hifadhi mayai penye hewa ya kutosha yasiharibike
- Mtunze kuku anayeatamia mayai (mpe chakula kidogo na maji)
- Kuku aatamie mayai yanayomtosha kulingana na ukubwa wake (mayai 8-12)
- Tunza vifaranga (chakula cha ziada, maji, kinga na wanyama/ndege, kinga na ajali)
- Kinga kuku na magonjwa
    - Chanjo ya mdondo/kideri
    - Madawa ya wadudu hasa viroboto (mfano ***Sevin dudu dust***)
    - Madawa ya minyoo
- Ongeza idadi ya kuku kadri ya uwezo wako
- Zingatia idadi ya majogop isiwe kubwa sana (jogoo mmoja kwa majike 8-15)
- Uza kuku jinsi wanavyoongezeka ili kubainisha faida ya ufugaji
- Tafuta ushauri wa kitaalamu kila inapobidi; hasa juu ya ujenzi wa banda, lishe, kudhibiti magonjwa na soko la uhakika

## Kiambatisho Namba 6: Matarajio ya washiriki

| Tarajio | Wakulima | Watafiti | Wagani | Taasisi |
|---|---|---|---|---|
| 1. Kupanua elimu ya ufugaji wa kuku wa kienyeji | 11 | 1 | 1 | 1 |
| 2. Kuweka mkakati wa uboreshaji wa uzalishaji na pato kutokana na kuku wa kienyeji | | 1 | 3 | |
| 3. Kupata ufumbuzi wa matatizo ya kuku hasa magonjwa | 3 | 1 | 1 | |
| 4. Kuelewa matizo katika utunzaji, magonjwa na uuzaji wa kuku wa kienyeji | 1 | 3 | 1 | 1 |
| 5. Kujua namna ya kuboresha kuku wa kienyeji | 5 | 2 | 2 | |
| 6. Kubadilishana uzoefu | 2 | 1 | 1 | |
| 7. Kujua nafasi anayopewa kuku wa kienyeji katika uchumi | | 1 | | |

Matarajio hayo yalithibitisha kuwa washiriki walitoka makwao wakiwa na ari ya kushiriki katika warsha hiyo kwa vile matarajio yao yanakwenda sawia na mada ya warsha.